# TARAJIO

Asante sana, ndugu, nami nina furaha kuwa hapa. Bwana na awabariki. Mwaweza kuketi sasa ndipo tutaninii . . .

2 Bila shaka nina majaliwa makubwa asubuhi ya leo kusimama mimbarani hapa Tucson kwa mara yangu ya kwanza maishani. Nilikuwa nikiwazia, nilipokuja huku asubuhi ya leo, kwamba ni miji mingapi kote ulimwenguni ambayo Bwana amenipa majaliwa ya kuitembelea, na kuzungumza na makusanyiko, na asubuhi ya leo ikiwa ndiyo mara yangu ya kwanza hapa Marekani kuwa kwenye jiji hili zuri.

3 Tangu tumekuwa hapa tumejifunza kuwapenda watu wake na—na mazingira yenu, hali yenu nzuri ya hewa, milima ya kupendeza, majangwa. Kuna jambo fulani juu yake, lingenifanya niwe na shauku ya kukaa hapa. Ni patulivu sana. Tulikuwa huko jangwani jana tukiangalia kote, na inaonekana tu kana kwamba unapokuwa huko nje kwamba Mungu anazungumza.

4 Hakuna kitu chenye haraka, hawaendi popote, hawasisimkwi juu ya chochote, kwa hiyo wao ni watulivu tu na wamestarehe. Na hiyo inaonekana sana sana kama watu wao niliokutana nao hapa: wamestarehe. Hakuna haraka, hatuko kwenye haraka ya kufanya lolote, na hapo ni mahali pazuri kwa ajili ya mhudumu mwenye wasiwasi, apate kutulia. Hakuna haraka. Maisha yametupatia "mkukumkuku mwingi," kama tusemavyo, "kwenda huku na huko," nasi hatuna budi kumalizia *hiki* katika dakika chache, na *hiki*, na kiasi fulani tu cha wakati. Inaonekana kana kwamba unapokuja hapa, "Vema, haraka ni ya nini?" Nami napenda hilo.

5 Na sasa, mnaweza kujifunza jambo lingine jangwani ambalo nafikiri kidogo ingefaa tuliangalie: miiba hiyo yote ya mpungate. Wakati mimi . . . Mnaona hizo sindano, wala siamini kungekuwako na mtambo ungaliweza kunoa moja ipate makali hivyo. Mwanangu angeweza kusema "amina" kwa hilo, maana ilitubidi kumtolea hiyo siku nzima jana. Na sasa, kama maskini mpungate huo ulikuwa—ulikuwa nchini mwangu, ungekunjuka na kuwa jani zuri jororo, kwa kuwa jambo ni kwamba, ni jani lililokunjamana. Nayo maumbile yakalinoa hivyo. Hivyo ndivyo unavyojilinda wenyewe. Huenda ikawa vema kwetu kuwazia hilo kwa dakika moja.

6 Sasa, weka maji kwenye jangwa hili na uyaache kwa miaka kadhaa, mpungate huo ungetokea ukiwa na majani, ungekuwa ni mwororo. Na hivyo ndivyo makanisa yanavyokuwa wakati mwingine tunapoenda bila maji ya kiroho. Tunajikunja sana na kuchomana mmoja na mwenzake. Lakini yamwagilie maji, nayo

yanalainika, na ni rahisi kubadilika, nami nafikiri hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa na makanisa, ni ambapo tunaweza kuwa na maji ya kiroho yanayotufanya watamu na wororo ili kwamba Mungu aweze kututumia; na wanaokukunjika kwa urahisi na pasipo kuchomana, lakini kulalia bega la jamaa huyo mwingine kwa upole na utamu, na kila mmoja wetu tukichukuliana mizigo na hivyo kuitimiza sheria ya Kristo.

7 Nilikutana na maskini mchungaji wenu, na ilikuwa ni mara yangu ya kwanza maishani kukutana naye, na ni jamaa mzuri sana. Ninashukuru kwamba analo kanisa hili zuri sana hapa na kusanyiko hili. Halafu rafiki yangu mwema, mmoja wa wafuasi wenu hapa Ndugu Norman, Dada Norman ambao. . . walikuwa wageni pamoja nanyi lakini sasa wemekuwa wenyeji, nafikiri, wa kuishi. Siwalaumu. Naye aliniambia, "Wakati tukilijenga kanisa hili," alisema, "wakati nilipopigilia hatua ya mwisho, msumari mle ndani," kasema, "nilisema, 'Ee Mungu, jalia rafiki yangu, Ndugu Branham, apande vipandio hivi siku moja na kulihubiria hili kusanyiko.'" Naye alikuwa amesimama kule nyuma akilia juu yake dakika chache zilizopita, jinsi ambavyo Mungu alikuwa amejibu maombi yake.

8 Nami ni—ninashukuru sana kwa ajili ya majaliwa ya kuwa hapa. Nime. . . Ninyi ni watu. . . Nilikutana, jambo pekee ninalojua kumwita ni Ndugu Tony, nisingeweza kulitamka jina hilo la Kitaliano. Na kwa hiyo nilikutana naye, naye ni mtu mzuri. Na mtu mwingine, ninaamini wanamwita Otto—Otto, Otto—Otto, kitu kama hicho. Mimi si mzuri sana kwenye haya, kuyatamka majina. Um-hum.

9 Nasi tulikuwa na kongamano la kimataifa jana. Kulikuwako na Mjerumani kule, na Mwitaliano, na wowote wale, na—nami nilikuwa huko kama Mwairishi. Kwa hiyo nikasema, "Hili ni kongamano la kimataifa." Wengi wa hao wavulana, baadhi yao walikuwa katika nchi za ng'ambo wakipigana na mataifa, na kadhalika, pamoja na mataifa mbalimbali. Lakini kama wote wangeweza kujisikia kama tulivyojisikia jana tukisimama kule jangwani, kusingekuwako na vita tena; tungekuwa ndugu. Kristo ndiye Jibu.

10 Nikiliangalia bonde hili la kupendeza na milima inayolizunguka, mirefu sana, nalipenda. Nilikuwa nimeketi kule juu sana, nikiangalia chini juu ya. . . jiji hili nami nikawazia, "Ni watafuta madini wangapi katika siku zilizopita wamepitia juu ya ardhi hii na kuangamia mumu humu jangwani, wakitafuta mgodi wa dhahabu?" Nazo siku hizo ni kama tu zimepita sasa, bali tunamshukuru Mungu tumepata mgodi wa dhahabu. Hamwichimbi kutoka kwenye vilima vyenu hapa; mnaipata huko juu angani. Na sasa, siku hizi hatutafuti madini tena, bali "tunamshuku" Mungu apate kutimiza kila ahadi aliyowahi kufanya, na kutumwagia baraka Zake nyingi.

11 Naye anabaki Mungu, nao moyo Wake una shauku ya kutupa tuombayo, kadiri tuombayo, na zaidi sana: kwa sababu "Yeye aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee; kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele." Na ikiwa alitupenda tulipokuwa tungali wenye dhambi, tumetenganishwa Naye, jumuiya ya Mungu, ni zaidi sana vipi Yeye yuko radhi asubuhi ya leo kutupatia kwa wingi sana zaidi ya yote tungaliweza kufanya au kuwazia.

12 Nasi tunakuja mjini kutembea. Tunaondoka kesho sasa kwenda California, tukwee hata sehemu ya kaskazini, na sehemu mbalimbali za ulimwengu. Lakini hakika ni majaliwa makubwa kwangu kusimama hapa asubuhi ya leo kwenye kanisa hili la kupendeza, Assemblies of God. Wamekuwa ni baadhi ya wadhamini wangu wakuu, kote duniani. Watu wazuri ni wafuasi wa dhehebu hili, wahudumu wazuri, walei wazuri. Nafikiri watu wote wa Mungu ni wazuri; popote unapowapata, ni watu wazuri.

13 Na nikiwa mmishenari na kusafiri sana, yapata mara saba kote duniani, ninakuta ya kwamba Roho Mtakatifu... Ukiingia, tuseme, Tailandi, Japani, Afrika Kusini, ukarudi nyuma huko kwa Wahotentoti, na sehemu hizo huko, ambako wanaume na wanawake wanakuja kanisani bila kuvaa kipande kimoja cha nguo, kwa sababu hawajui tofauti. Makumi ya maelfu wao wanakaa pamoja. Kama u—kama ungeweza kuzungumza lugha yao, useme, "Mkono wa kulia ni upi, na wa kushoto?" wasingejua ulichokuwa ukizungumzia. Yote wajuayo ni kuua kile wanachoweza kula; iwapo hawawezi...njia yoyote unayopata chakula; ni kuendelea kuishi, kama tu vile mnyama angefanya.

14 Lakini kunalo jambo moja linalowafanya wawe sisi. Ukisimama katika kusanyiko kama hilo na kumwacha Roho Mtakatifu awashukie, wanafanya jambo lile lile ufanyalo unapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda vivyo hivyo. Inaonyesha ya kwamba Mungu hana upendeleo wa watu wala taifa. Kama vile Matendo 4 isemavyo, ya kwamba Petro alisema aliona ya kwamba Mungu hana upendeleo wa taifa lolote, bali wote wamchao. Na kwa hiyo tuna kitu fulani shirika: hicho ni Yesu Kristo.

15 Nilimpigia simu mke wangu muda mfupi uliopita na ni karibu sufuri kule; na hata shule zimefungwa na theluji, zote zimefunikwa na theluji, nazo barabara zinateleza sana. Kama mtu yeyote ametoka Mashariki, afadhali ufurahi uko huku Magharibi sasa, maana ni baridi sana. Kwa hiyo tusingeweza kuwa na vitu shirika kwa nchi yangu na nchi hii, bali tunavyo pamoja na Mungu wangu na Mungu wako, kwa sababu ni Mungu yeye yule.

16 Nimekuja asubuhi hii kidogo kuitambulisha huduma ambayo Bwana Yesu ameniruhusu kuieneza kote ulimwenguni.

Nami niliwazia, asubuhi ya leo katika shule ya Jumapili, ingewapa watu na—nafasi ambapo ningeweza kuwaelezea, kwa kuwa tupo hapa usiku mmoja tu, ili kwamba, wapate kumpokea Kristo kwa ajili ya uponyaji wa mwili wao. Na mambo madogo ya kipekee, mara ya kwanza kuwa hapa, jambo fulani huenda likaonekana la kigeni kidogo kwenu. "Kwa nini wakalifanya hivi? Kwa nini hawakulifanya hivi vingine?" Huenda nikaelezea hilo.

17 Sasa, kwa kawaida tunapoingia kwenye mji wakati tukiwa na mkutano mkubwa, mbona, tu—tunaomba ushirikiano na ushirikishaji wa makanisa yote kukutanika pamoja, kusudi Kristo asiwe amegawanyika miongoni mwetu; Yeye ni Kristo yule yule miongoni mwetu sote. Nasi tunajaribu kuleta madhehebu yote, Methodisti, Baptisti, Pentekoste, Church of God, Holiness, na wote, pamoja. Ndipo tunaketi pamoja mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, pamoja na matarajio ya kwamba Mungu ataimwaga Roho Yake juu yetu na kufanya "mambo makuu sana." Sasa, kisha tunapofanya hivyo. . .

18 Daima nimetoa tamshi hili: mimi. . .Kila mmoja anajua ya kwamba nilikuwa Mbaptisti wa Kimishenari, nami ni Mbaptisti wa Kimishenari aliyempokea Roho Mtakatifu. Kwa hiyo basi katika hilo, siamini ya kwamba Pentekoste ni dhehebu. Ninaamini Pentekoste ni tukio ambalo yeyote atakaye anaweza kuja na kupokea. Hatuwezi kuweka ua kuizunguka, kwa kuwa sivyo ilivyo, inasambaa kupita nyua zetu, mnaona.

19 Kwa hiyo ninaamini ya kwamba mtu ameokoka (kama ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, ama chochote alicho) kama kabisa anamtumainia Yesu Kristo kwa ajili ya neema Yake. Lakini iwapo yeye ni Mkatoliki na anaamini kanisa humwokoa, basi amepotea. Iwapo ni Mpentekoste na anaamini kanisa humwokoa, amepotea. Lakini haidhuru yeye ni nani, kanisa analohudhuria, kama anategemea Damu na ustahilifu wa Yesu Kristo kwa dhati, ameokoka, sijali yuko katika kanisa gani. Kwa kuwa tunaokolewa kwa imani, hiyo ni kwa neema.

20 Nilikuwa nikiwachunga ng'ombe, ninawapeleka kwenye mikusanyiko huko Colorado na huko kwe—kwenye Bonde la Troublesome River, Shirika la Hereford hulishia kwenye bonde hilo. Nadhani mna sheria zizo hizo hapa, na kupata cha—chapa, kumbukumbu ya Chama cha Wafanyabiashara na kadhalika. Basi iwapo unaweza kuchangia tani moja ya nyasi kavu shambani mwako, vema, basi unaweza kuwatuma ng'ombe wako ndani kwa, ng'ombe mmoja kwa tani moja ya nyasi kavu hiyo ranchi itatoa, kwa ajili ya haki za ulishaji mwituni.

21 Wana uzio wa kuwadhibiti ng'ombe ambapo tunapanda Troublesome River, Mkondo wa Magharibi, Mkondo wa Mashariki, wa Troublesome River. Na mara nyingi nimeketi pale asubuhi katika mkusanyiko wa msimu wa kuchipua,

nikiwapandisha hao ng'ombe, nikaweka mguu wangu kuikingama pembe ya matandiko, huku nikimwangalia mhifadhi amesimama pale, akiwakagua hao ng'ombe wakipita. Siku moja nikiketi pale, niliwazia, "Hivi ndivyo itakavyokuwa huko Mbinguni tutakapofika kwenye lile lango kuu."

22 Nami niliwaona wakipita pale, kulikuwako na yapata chapa kumi na tano ama kumi na sita mbalimbali za hao ng'ombe wanaoingia mle. Baadhi yao ni Mkuo wa Almasi, hao ni wa Bw. Grimes huko juu kwenye ranchi; Bw. Jeverez, Mburuzo wa Batamzinga; na—na chapa mbalimbali. Mhifadhi hakuwa akiiangalia chapa sana. Hakuwa akiizingatia sana hiyo; bali alikuwa akiangalia kile kibandiko cha damu sikioni, maana huwezi kumweka ng'ombe kwenye malisho hayo isipokuwa awe ni Herefodi ukoo safi. Na hiyo ndiyo wanayotaka kuelewa, ya kwamba wao ni ukoo safi, iliwabidi wachunguzwe damu.

23 Nikawazia, "Hivyo ndivyo itakavyokuwa hasa kwenye Siku ya Hukumu. Yeye hataona nimebandikwa chapa gani, kama mimi ni Mbaptisti ama Mpentekoste ama Mpresbiteri, bali ataangalia ile Damu, kile kibandiko cha Damu. 'Nitakapoiona hiyo Damu, nitapita juu yenu.'" Tunaingia kwa kile tulicho; si kwamba sisi ni nani.

24 Sasa, tutakapokuja kwenye ibada usiku wa leo, ibada huanza kama saa ngapi, Kasisi. . .?. . .Saa moja na dakika arobaini na tano, basi yapata saa kumi na mbili na nusu, nadhani, kati ya saa kumi na mbili na saa kumi na mbili na nusu nitawatuma wengine huku chini kuwapa watu kadi za maombi, kidogo kabla ya ibada hiyo, kwa hiyo hawataikatiza ibada inapoanza. Nao wagonjwa na waje hapa mbele kusudi niwe karibu kabisa nao. Halafu kutakuwako na kadi ya maombi; huyo mvulana atakuja na kuleta kadi nyingi, na kuzichanganya zote hapa mbele yenu, kisha kumpa tu kila mmoja kadi ya maombi (Mnaona?) mtakazo. Kila mmoja anayetaka kadi ya maombi, waweza kuipata.

25 Kwa hiyo, sababu ya sisi kufanya hivyo. . .Ilikuwa kwamba tungetuma mkutanoni ninii kadhaa. . .Kila mchungaji aliyeshirikiana, tungemtumia kadi mia moja kwa ajili ya kusanyiko lake. Vema, wa kwanza kuliingiza kundi lake, hilo lilitosha. Hao wengine hawakuingia, maana, tukiwa pale labda yapata siku tatu usiku, nisingeweza kuipitisha idadi hiyo ya watu kwenye mstari wa maombi. Ndipo tukaona kwamba hilo lisingefanya kazi.

26 Kwa hiyo basi, nikapata baadhi. . .mhudumu kuambatana nami akasambaze kadi za maombi, naye alikuwa. . .alikuwa mfuasi wa dhehebu fulani; na wakati asingeonyesha upendeleo kidogo kwa dhehebu lake mwenyewe, vema, basi kidogo hilo likasababisha hamaki.

27 Kwa hiyo basi, kwa kawaida mimi huwaita watu kumi ama kumi na watano jukwaani kwanza. Vema, iwapo hawakuwa na kadi ya maombi namba moja hadi kumi na tano, mbona, wangeitupa tu sakafuni. Hawakuitaka, maana hawataitwa. Kwa hiyo tukaona hilo halingefanya kazi.

Ndipo ningemchukua mtoto, kama mmoja wa hao wavulana wadogo, nami ningesema, "Hebu njoo hapa juu, mwanangu, ama msichana mdogo, tuseme, ameketi pajani mwa mama yake."

Ningesema, "Unaweza kuhesabu?"

"Naam, bwana."

"Basi anza kuhesabu."

Vema, angeanza, "huru, nne, tano, sita," mpaka ambapo alisimamia; ningeanzia papo hapo.

28 Vema, amini usiamini, tungali tuna wanadamu; mama alijua mahali pa kumwambia Kadogoo mahali pa kusimama kwa ajili ya kadi yake. Kwa hiyo tukaona hilo halitafanya kazi.

29 Kwa hiyo basi, basi tukampata mtu kwenye mstari wa maombi, ama juu wakati mmoja, akiuza kadi za maombi kuwatanguliza watu jukwaani. Kwa hiyo hilo lisingefanikiwa.

30 Kwa hiyo usiku mmoja Bwana akanifunulia kumwacha mtu ashuke aje akasambaze kadi za maombi, na kusimama mbele ya kusanyiko na kuzichanganya zote. Ndipo huenda huyu akapata namba moja, huyu thelathini na tano, na yule sitini na mbili, na huyo anayemfuata. Zote zingechanganywa. Ndipo basi hiyo ingeonyesha ya kwamba huyo mtu aliyekuwa akizisambaza kadi za maombi hakuwa ndiye aliyewaweka hapa juu, maana yeye hakujua. Zote zilikuwa zimechanganyikana.

31 Halafu, hata hivyo, ninapokuja mkutanoni, vema, wakati mwingine ningeanza kwenye namba moja, mara nyingine ishirini na tano na hamsini. Wakati mwingine nitachukua idadi ya waliokuwa wameketi kwenye kiti hiki (mimi binafsi, wakati nikizungumza), kisha nizidishe na hii ya upande huu mwingine, na, loo, njia yoyote ile. Hivyo inaliacha huru kwa kusanyiko zima. Na jambo lingine, kuna yapata hamsini wanaoponywa kwenye kusanyiko kwa mmoja anayeponywa jukwaani.

32 Ujumbe sio kujaribu kumponya mtu fulani, kwa sababu uponyaji ni kitu ambacho tayari kimenunuliwa. Wokovu umenunuliwa. Kamwe hukuokoka tu juma lililopita, ama mwaka uliopita, ama miaka mitano iliyopita; uliokolewa wakati Yesu alipokufia pale Kalvari. Huo ulikuwa ndio wokovu wako; na sasa, ndio kwanza uukubali majuma mawili yaliyopita, ama miaka miwili iliyopita, chochote kile. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa, kuponywa: Sisi. . . "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake tuli-," wakati uliopita, "tuliponywa." Kwa hiyo ni kuwafanya tu watu waone, watambue, ya kwamba

Uwepo wa Kristo uko karibu. Hilo ndilo linaloleta matokeo ya maelfu ya watu kuponywa.

Sasa, kabla tu hatujalikaribia Neno, hebu tumkaribie Mwandishi, kwanza, katika maombi mafupi wakati tumeviinamisha vichwa vyetu.

33 Baba yetu wa Mbinguni mwenye neema, tunaukaribia utakatifu Wako asubuhi ya leo, katika Jina litoshelezalo kwa yote la Yesu Kristo, Mwana Wako, kwa sababu tumefundishwa Naye katika Neno ya kwamba tukiomba Baba lolote katika Jina Lake litajaliwa. Hatuna jina lingine ambalo tunaweza kuwa na hakika ya kwamba Yeye atatusikia, ila tu kwa Jina hilo litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu.

34 Tunakushukuru Wewe, kwanza, Baba, kwa yale ambayo Wewe umetufanyia tayari, zile baraka nyingi, neema kuu ambayo Wewe umetukirimia. Na halafu tunakushukuru kwa ajili ya neema tuliyo nayo asubuhi ya leo kusimama katika kanisa hili jipya, ambalo ni kumbukumbu iliyojengwa hapa jijini, likasimamishwa hapa kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kusudi wenye dhambi waliopotea waweze kuingia na kuokolewa; ambapo wagonjwa, waliopita madaktari, matabibu wa duniani, wamepita ufahamu wao, kwamba wangali wanaweza kuja kwenye nguvu kuu zaidi, Mwenyezi, na kuponywa. Loo, jinsi tunavyokupenda Wewe daima, Baba. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya haya.

35 Nasi ni watu waliojaliwa kuwazia juu ya Warusi asubuhi ya leo pamoja na hizo Sputniki kubwa huko juu angani zikiwa na mtu ameketi ndani yake, na kusikia mpigo wake wa moyo kote kote hata duniani. Jinsi mwisho ulivyo karibu hapa! Unalijilia hili taifa na ni "Jisalimisheni la sivyo mwangamie!" Na, Ee Mungu! Wazia jinsi ingekuwa kama kamwe wangeanza kurusha hayo makombora. Maskini hii dunia ingetikisika iingie angani, na hapatakuwapo na wakati baada ya hayo.

36 Lakini tumefundishwa katika Neno lililobarikiwa, kabla hili hata halijatukia, Kanisa linaenda Nyumbani kuwa pamoja na Bwana wake. Loo, jinsi Nuhu alivyoingia safinani kabla mvua haijanyesha; Lutu aliitwa atoke Sodoma kabla moto haujashuka. Bwana, tunaamini Kanisa litanyakuliwa kutoka humu duniani kabla yale maangamizi makuu hayajaja. Tuna furaha sana kujua tuko karibu na wakati huo.

37 Na, Baba, tunapoangalia asubuhi ya leo na kujua ya kwamba lingetukia kabla ya usiku, taifa hili, ama ulimwengu, ungeweza kulipuliwa vipande-vipande. Taifa dogo ama mshupavu fulani akiachilia moja ya makombora hayo nayo yote yameelekezwa moja kwa lingine, hapa lingeenda; ila kabla hilo halijatukia, Mungu, kule Kunyakuliwa, parapanda italia nasi tutaitwa angani kumlaki Bwana wetu. Tunapaswa kuwa watu wa aina gani asubuhi ya leo? Wenye furaha, tukiinua vichwa vyetu

tunapouona mtini ukichipusha, na zile ishara kuu, na sayansi ikisema ni dakika tatu kabla ya usiku wa manane. Karibu wakati wowote lingeweza kupiga.

38 Ee Mungu, lipige kanisa asubuhi ya leo, Bwana, kwa nguvu Zako na kwa hekima Yako kuu. Lipige leo, na ujalie mbawa Zako kuu zienee kote kwenye jengo hili dogo leo; na uwachukue watoto kule chini kama kuku awafanyiavyo vifaranga vyake, kisha uwashughulikie wagonjwa wapate afya tena, kimwili na kiroho. Lijalie, Bwana. Libariki kanisa hili. Bariki kusudi linalosimamia hapa, kusudi linalowakilisha: mchungaji, wazee, mashemasi, wadhamini, na walei, na wageni wote malangoni petu.

39 Sio tu kwa kanisa hili, bali tunaomba ya kwamba Wewe utalibariki kila kanisa kote nchini. Na kwa sababu ya kusanyiko hili dogo leo hii, jalia kuibuke uamsho wa mtindo wa kale ambao utasambaa Arizona hii kutoka upande mmoja hadi mwingine. Lijalie, Bwana. Kwa unyenyekevu tutainamisha vichwa vyetu Mbele Zako na kutoa shukrani, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwana Wako mpendwa, Mwokozi wetu. Amina.

40 Sasa, sio kuhubiri, bali ni kuweka tu utaratibu kidogo, kuiandaa mioyo kwa ajili ya tukio la usiku wa leo, ambapo tunaamini ya kwamba Baba yetu wa Mbinguni atakutana nasi. Halafu labda kwenye wakati ufaao, Bwana akipenda, tungetaka kurudi labda kwa muda mrefu zaidi, ambapo tungeweza kukutanika pamoja, na kuwakusanya ndugu pamoja. Tuko tu matembezini.

41 Lakini ningetaka kusoma kutoka Luka Mtakatifu, mlango wa pili na kifungu cha 25, kifungu cha 26:

> *Naye alikuwa ameonyeshwa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti* mpaka *amemwona Kristo wa Bwana.*

42 Nitatumia somo la *Tarajio*. Matarajio kwa kawaida yamewekwa msingi juu ya imani. Inakupasa kuwa na imani kabla ya kuweza kutarajia chochote. Na sasa, kama vile wengi wa watumishi wa Mungu katika Agano la Kale: “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.”

43 Na mara nyingi nimenukuu hili, ya kwamba Mungu anawajibika kwa Neno Lake. Ninapenda kusoma neno moja tu ama mawili Yake, kwa maana nisemayo yatashindwa, kwa sababu mimi ni mwanadamu, bali Neno Lake haliwezi kushindwa kwa sababu Hilo ni Mungu. Yale. . .Mungu kamwe akiitwa jukwaani wakati wowote kufanya u—uamuzi, basi uamuzi wa kwanza anaofanya Mungu, hauna budi kuwa ni uamuzi ule ule kila wakati.

44 Sasa, hapo ndipo huna budi kuiweka imani yako msingi kwa dhati, juu ya BWANA ASEMA HIVI. Huna budi kuliamini, ya kwamba ni Neno la Mungu. Na hilo ndilo tumaini pekee

tulilo nalo, tumaini thabiti pekee tulilo nalo, ni juu ya Neno la Mungu. Na sasa, Mungu akiwa ni asiye na kikomo, wala hawezi kufanya kosa, Naye ni mkamilifu, kwa hiyo, ninii Yake yote—ahadi Zake zote hazina budi kuwa kamilifu kama vile Yeye alivyo mkamilifu. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu," Neno Lenyewe, kwa hiyo basi, Biblia ni Neno la Mungu. Ni Mungu Mwenyewe amewekwa juu ya karatasi.

45 Kwa kuwa hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake. Kama siwezi kulichukua Neno la mtu, kamwe siwezi kuwa na uhusiano wowote naye. Hana budi kuwa mwaminifu, hana budi kuwa mkweli, na hasa sana wakati akikiri kuwa Mkristo.

46 Sasa, hilo ni fungu dogo fupi tu, bali si kwamba ni kiasi gani. Sio ule ubora, ama, ukubwa; ni ubora wa Neno. Ni kile lilicho: Ni Neno la Mungu.

47 Simeoni hapa, wa kale, alisema kwamba iliahidiwa na Roho Mtakatifu kwamba hataona mauti mpaka atakapomwona Kristo wa Bwana. Alikuwa na haki ya kulitarajia, kwa sababu Mungu alikuwa amemfunulia kwa Roho Mtakatifu. Alikuwa na sababu ya kulifunua.

48 Sasa, tunaona ya kwamba Ibrahimu wa kale, alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano naye mkewe sitini na mitano, Sara, jinsi ambavyo Mungu alisema naye na kumfunulia ya kwamba atampata mtoto kwa Sara, mkewe. Alikuwa tasa naye mke alikuwa mgumba. Nao walikuwa jinsi hii maishani mwao mwote, bali hata hivyo Mungu akamwambia atampata mtoto kwa Sara. Ndipo akamwambia ajitenge kwa sababu ya ahadi hii.

49 Na hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya: Tunapoliamini Neno la Mungu, hatuna budi kujitenga na mambo yote yanayokuzunguka ambayo ni kinyume na Neno hilo. Huwezi kuwaendea watu na kusema, "Sasa, unafikiri nimepata uponyaji wangu? Unafikiri. . .?" Si yale wanayowazia; hilo halina uhusiano wowote katika hilo. Ni yale unayofikiri wewe. Ni juu yako. Kwa hiyo aliombwa kujitenga mwenyewe, naye akafanya hivyo kwa matarajio makuu ya kumpokea yule mwana.

50 Sasa, tunaona ya kwamba mtoto huyo kamwe hakuwasili mpaka miaka ishirini na mitano baadaye. Lakini badala ya kuwa mnyonge kwa kuwa halikutukia mwezi wa kwanza, yeye alipata nguvu zaidi wakati wote, kwa kuwa matarajio yake yalikuwa ni makuu zaidi. Kama Sara alikuwa mwezi mmoja mzee zaidi, ingekuwa kuu mwezi mmoja zaidi katika hayo matarajio, kwa sababu Mungu alilitimiza Neno Lake. Ingekuwa ni afadhali zaidi kumpata huyo mtoto kwenye umri wa miaka mia moja kuliko ingalikuwa kwenye umri wa miaka sitini. Mnaona ninalomaanisha? Ulikuwa ni mwujiza mkubwa zaidi

wakati wote. Wala hakuwa mnyonge, bali alipata nguvu zaidi wakati wote.

51 Sasa, sisi ni watoto wa Ibrahimu, Biblia ilisema hivyo. Sisi, tukiwa tumekufa katika Kristo, tunachukua uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi sawasawa na ile ahadi. Sisi ni warithi wa ile ahadi pamoja na Ibrahimu, kwa sababu Ibrahimu alipewa ile ahadi. Sasa, kama sisi ni warithi wake pamoja na Ibrahimu, basi sisi ni wana wa Ibrahimu. Nayo imani ile ile aliyokuwa nayo Ibrahimu, tunayo sisi wenyewe, kwamba wakati Mungu anapofanya ahadi, jua tu itatimia. Haiwezi kufanya jambo lingine lolote.

52 Ungeweza kuwazia Ibrahimu akitoka nje, akienda...? Tuseme tu alienda, yeye na Sara. Alikuwa na sabini na mitano naye mke sitini na mitano, hiyo ni yapata miaka kumi na mitano, ishirini baada ya kukoma hedhi. Naye alikuwa ni dada yake wa kambo. Alikuwa ameishi naye tangu alipoolewa naye kwanza, labda kwenye umri wa miaka kumi na sita ama kumi na saba, na bila watoto. Ndipo Mungu akamtokea na kumwambia atapata mtoto. Sasa, Ibrahimu alitarajia hilo litukie, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

53 Ningeweza kumwazia kwenye...Ungeweza kumwazia mzee mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mwanamke sitini na mitano, wakishuka kwenda kumwona daktari kufanya... kufanya maandalizi pamoja na hospitali wakamzae mtoto? Watu wangewaambia nini? Daktari angesemaje? "Huyo jamaa mzee ana ki-...ana kasoro kiakili. Jamaa huyo mkongwe yuna kasoro." Vema, kila mwanamume ama mwanamke anayemchukua Mungu kwa imani, na kuzikubali ahadi Zake, anahesabiwa na ulimwengu huu namna fulani ya mwendawazimu ama mlokole, kwa kuwa mambo ya ulimwengu huu ni upumbavu sana kwa Mungu. Kile mwanadamu anachokiita kikuu, Mungu hukiita kijinga. Sasa, bali Ibrahimu aliliamini.

Sasa, siku za kwanza ishirini na nane baadaye (yeye akiwa amekoma hedhi kwa yapata miaka kumi na mitano, ishirini): "Unajisikiaje, Mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

"Vema, Mungu asifiwe, tutampata huyo mtoto haidhuru."

54 Ilikuwa ni matarajio makubwa sana, labda Sara alishona vijibuti vidogo, na blanketi ndogo, na...Kwa nini? Alikuwa akitarajia jambo fulani litukie, hiyo ndiyo sababu lilitukia. Mwaka baada ya mwaka ulipita, naye Ibrahimu akazidi kupata nguvu zaidi na zaidi, akimsifu Mungu. Ndipo hatimaye likatukia, kwa maana alilitarajia litukie.

Akiisha kupata umri wa miaka tisini ama, yeye alikuwa na tisini: "Unaonaje sasa kulihusu, Ibrahimu? Uko karibu kukata tamaa?"

"La, bwana, tutampata huyo mtoto haidhuru. Tayari tumeweka nguo akiba, tumeandaa kila kitu."

"Mmekuwa nazo muda gani?"

"Miaka ishirini na mitano, bali Mungu atamtuma huyo mtoto kwa vyovyote vile."

55 Ninapenda jambo hilo. Mnaona, ni hakika. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha. Mungu anapofanya uamuzi, Yeye hana budi kuufanya wa Milele. Sasa, naweza kufanya uamuzi, na dakika tano inilazimu kurudi na kufanya mwingine, maana nilikosea katika huo. Unaweza, pia, kwa kuwa sisi tuna kikomo. Lakini Mungu, akiwa hana kikomo, hawezi kukosea. Yeye ni Mungu asiyeweza kukosea, mwenye nguvu zote, anayeenea kote, asiye na kikomo. Amina. Wakati uamuzi Wake unapofanywa, umekamilika milele. Yeye hawezi kurudi na kusema, "Nilikosea." Hawezi kufanya hivyo.

56 Na kama Mungu alifanya uamuzi hapo mwanzo juu ya imani, kama tuliliamini Neno Lake, Yeye angefanya kila ahadi iwe ni kweli, ndipo Mungu angali ni Mungu asiye na kikomo kwa ahadi Zake. Haiwezi kushindwa, haina budi kuwa hivyo. Ni ya hakika. Inakubidi kufikia mahali hapo kama utalichukua Neno Lake, uliamini.

57 Sasa, kama Yeye angalisema . . . Vema, kama vile makanisa yanavyosema kwamba, sio . . . wahudumu fulani husema ya kwamba siku za miujiza zimepita; Mungu hawaponyi watu tena. Kama Mungu alipata kuitwa jukwaani kwa mtu mgonjwa naye akamponya juu ya msingi wa imani yake, kama mgonjwa mwingine akimjia, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile, la sivyo alikosea wakati alipomponya mtu wa kwanza.

58 Kama alimpa mmoja Roho Mtakatifu ambaye alimtii, katika Biblia, jinsi hasa alivyoahidi pale katika Matendo . . . Yeye alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, hao walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Kama mtu huyo akitimiza masharti hayo, Mungu anawajibika kwa Neno Lake kumjaza na Roho Mtakatifu, kwa sababu kama hakufanya hivyo, basi—basi Yeye alifanya kosa. Na kama Mungu alifanya kosa, Yeye ni mwanadamu wala si—si Mungu. Yeye—Yeye yuna kikomo, kama tulivyo sisi. Kwa hiyo unaona, kama watoto wa Ibrahimu tunaichukua ahadi ya Mungu na kuishikilia tu. Haijalishi ni jambo gani linalotukia, tunashikilia papo hapo vivyo hivyo, kwa sababu Mungu alisema hivyo na hilo latosha.

59 Sasa, huwezi kuudanganyia; huna budi kuwa nao. Hu—huwezi kuudanganyia. Hautadanganya. Shetani si . . . yeye—yeye anajua kama unadanganya ama la. Lakini wakati hudanganyi, yeye anajua pia. Wakati kitu fulani kinapotia nanga moyoni mwako ambapo unajua ya kwamba ndivyo ilivyo, basi jambo fulani litatukia.

60 Ibrahimu aliamini hilo. Yeye alimwamini Mungu. Aliliamini Neno la Mungu na chini ya matarajio; alingojea miaka ishirini na mitano huku tarajio hilo likizidi kuwa kubwa zaidi na zaidi. Ndipo hatimaye huyo mtoto akazaliwa, kwa sababu alikuwa akilitarajia.

61 Akajitenga. Na kama utaangalia kile alichongojea, Mungu alimwambia ajitenge na jamaa zake wote, wala Mungu kamwe hakumbariki tena mpaka alipomtii kikamilifu. Maadamu—maadamu baba yake aliendelea kuandamana naye, mbona, huyo jamaa mzee alisababisha matatizo. Kisha akaandamana na Lutu, halafu Lutu akasababisha matatizo. Na—na yote hata alipojitenga mwenyewe, na kuondokea, kutokuamini kote kukaondolewa kwake, ndipo Mungu alishuka na kuzungumza naye, ndipo jambo fulani likatukia.

62 Basi tunapoondolea mbali kutoka kwetu maskini roho zote za kutokuamini, na kuliamini tu Neno la Mungu, na, "Sijali yale *Fulani-wa-fulani* aliyosema, ama *Fulani-wa-fulani* aliyosema, Mungu alitoa ahadi, ninasimama papo hapo." Ndipo Mungu ataanza kujibu.

63 Lakini kumbukeni, Yeye alimbariki, na akamhifadhi, na kadhalika, ama akamlisha, na akamwongoza mahali mahali; bali kamwe hakumbariki kikamilifu na kumpa ile ahadi mpaka alipojitenga kabisa na kila kitu kidogo cha ulimwengu. Akamwacha mpwa wake ashuke aende Sodoma kama alitaka, na hao wengine *hivi-na-vile*. Baba yake akafa. Ndipo Mungu akamwambia, "Amka na uangalie kote nchini. Nimekupa wewe yote. Angalia mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini." Nafikiri hiyo ndiyo njia. Kama kanisa, watu fulani, kamwe wakifikia mahali ambapo wanajitenga kabisa na mambo ya ulimwengu, basi unaweza kuangalia kupitia kila ahadi katika Biblia. Zote ni zako.

64 Ni kama tao kubwa mno. Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika tao. Watu wengine wanaingia tu kwenye hilo tao kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kasema, "Vema, mshukuru Bwana, niliingia. Mshukuru Bwana, nipo hapa."

65 Hilo silo. Kwangu mimi, Mungu alimwambia nini Ibrahimu? "Simama uangalie kote nchini. Yote ni mali yako." Hiyo ndiyo njia, wakati nilipoingia katika—katika Kristo, nilitaka kuangalia kila mahali. Sio tu kujua Yeye aliniokoa, bali nina kitu gani tena mle? Kama mtu fulani alinipa tao kubwa nami nikaingia ndani yake, ningetaka kukichunguza kitu hicho, nione kwamba nina nini. Hivyo ndivyo ilivyo na Wakristo siku hizi. Wanakosa kuangalia zile ahadi za Mungu na kuona ni za "yeyote atakaye, na aje." Kama mimi . . . kitu fulani juu kidogo, ningechukua ngazi ya vipandio nikakifikie, niangalie kwenye rafu niione mali yangu.

66 Ninyi Wakristo wakati mwingine hamwangalii, kuchunguza, mwione mali yenu. Uponyaji ni wenu, wokovu ni wenu, furaha ni yenu, amani; kila ahadi katika Biblia ni yenu. Wakati mtu amejazwa na Roho Mtakatifu, Mungu humpa hundi iliyoandikwa Jina la Yesu chini yake. Itume ndani. Usiogope kuiandika. Itume ndani, ndipo Yeye atashusha baraka Zake nyingi juu yako za yale aliyoahidi.

67 Musa tayari alikuwa amekata tamaa. Alikuwa amerudi upande wa nyuma ya jangwa, akiwachunga kondoo wa Jethro baba mkwe wake, wakati asubuhi moja, huko nyuma upande wa nyuma ya jangwa, aliona kichaka kikiwaka moto. Akaenda mbele za kichaka hiki, ingawa Musa alikuwa ni mwanathiolojia, kwa sababu alifunzwa katika hekima na mafunzo yote ya Wamisri, alikuwa ameambiwa na mama yake ya kwamba alikuwa ameitiwa kusudi fulani, na ujuzi wake wote wa kithiolojia ukawa si kitu kwake.

68 Wala siidhalilishi thiolojia—ujuzi wa kithiolojia, ila ninasema kamwe haitachukua mahali pa tukio hilo unalokutana nalo unapokutana na Mungu. Jambo fulani hutukia. Yeye anakuwa kiumbe kipya. Wakati mwingine inakufanya ufanye mambo ya kipekee kwa walimwengu.

69 Ninaweza kumwazia Musa kesho yake asubuhi, pamoja na Zipora ameketi juu ya nyumbu pamoja na m—mtoto Gershomu pajani mwake, akishuka kwenda kuiteka Misri, maskini fimbo kavu mkononi mwake kama fimbo ya kutembelea, masharubu yakipeperushwa pande zote mbili. Na, "Kwani unaenda wapi, Musa?"

70 "Nashuka kwenda Misri kuiteka." Uvamizi wa mtu mmoja; kama tu mtu mmoja akienda Urusi kuiteka. Mzee, umri wa miaka mia moja, mke wake ameketi juu ya nyumbu pamoja na m—mtoto, wakishuka kwenda kuiteka. Lakini ukweli ni kwamba, aliiteka, kwa sababu Mungu alifanya hiyo ahadi, naye Musa alikuwa akimtarajia Mungu kuitimiza ahadi Yake.

71 A—a—akawauwa Wamisri. A—alishuka kule wakati mmoja na kumwua mtu mmoja nje ya mapenzi ya Mungu, nalo lilikuwa ni doa mikononi mwake; akashuka wakati huo mwingine akaliua taifa zima, ilikuwa ni utukufu mikononi mwake; kwa sababu wakati mmoja Musa alikuwa akilitenda, na wakati huo mwingine Mungu alilitenda; hilo linaleta tofauti. Alikuwa akimtarajia Mungu kuwakomboa, kwa sababu, "Nimesikia vilio vyao; nimeona mateso yao na Mimi," kiwakilishi nafsi, "nimeshuka kuwakomboa, nami ninakutuma wewe, Musa, mahali Pangu." Hilo lilitosha.

72 Yeye ameyaona mateso yako. Amemwona daktari akisema, "Siwezi kufanya lolote zaidi kuuhusu." Yeye ameshuka katika umbo la Roho Mtakatifu kuchukua mamlaka, ikiwa tu utamruhusu kufanya hivyo. Kuwa ukimtarajia kufanya hivyo,

jua ya kwamba Yeye aliahidi kufanya hivyo, lishikilie Neno Lake. Yeye alisema atafanya hivyo, kwa hiyo uwe ukilitarajia.

73 Simeoni, mtu mwenye sifa kubwa, Simeoni alikuwa mzee mwenye hekima, naye alikuwa ni. . .alikuwa na sifa kubwa miongoni mwa watu, kama uliwahi kuisoma katika historia yake; na yeye—yeye alikuwa ni mtu mheshimiwa. Nanyi mngeweza kuwazia mzee pale, karibu na umri wa miaka themanini na kitu, akienda huku na huku akisema, "Vema, mnajua sitakufa mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana."

74 Ninaweza kuwazia baadhi ya marabi wakisema, "Mnajua, maskini huyo mzee, inahuzunisha. Mbona, huyo mzee kidogo amerukwa na akili. Mbona, tumekuwa tukimtazamia Masihi kwa muda wa miaka elfu nne. Tangu Edeni watu wetu wamemtazamia Masihi; nasi hawa hapa katika utumwa wa Kirumi. Hali zote za mambo zimefungwa, ushahidi wote ya kwamba mambo haya yatatimia umefungiwa macho yetu; tuko utumwani. Sisi hata si taifa tena; tumevunjika-vunjika jinsi tulivyo, na chini ya serikali ya Kirumi. Na hapa mzee huyu mwenye mguu mmoja kaburini na huo mwingine ukiegemea, na hata hivyo anasema atamwona Kristo wa Bwana. Loo," wangesema, "jamani, hilo kamwe halitatukia."

Bali Simeoni alijua ya kwamba litatukia.

75 Ninaweza kuwazia baadhi ya marabi vijana wakisema, "Vema, achaneni tu na maskini mzee huyo. Hana madhara; hatamdhuru mtu yeyote. Lakini anaenda huku na huku akimshuhudia kila mtu hatafanya *hili*, na atafanya *lile*, naye ataishi apate kumwona Masihi akija, na yote namna *hiyo*."

76 "Vema, Simeoni, sababu yako ni ipi? Kwa nini unasema jambo kama hilo? Ni kitu gani kinachokufanya kusema, wakati Daudi alimtazamia, wakati Eliya alimtazamia, na wale manabii wa kale, nasi tulimtazamia kote katika kila wakati, na sasa siku za miujiza zimepita na kila kitu kimeingia giza, miaka mia nne tangu tulipokuwa na nabii, Malaki, nawe huyu hapa, unakuja, ukisema hutaona mauti hata utakapomwona Masihi, unajuaje hilo litakuwa ni kweli?"

"Kwa kuwa ilifunuliwa kwangu na Roho Mtakatifu."

77 Huo hapo msingi wake. Huo hauna budi kuwa ndio msingi wako. Huo hauna budi kuwa ndio msingi wangu. Wakati Roho Mtakatifu anapotufunulia na ni kulingana na Neno, hakuna kitu kitakacholikomesha, wakati imefunuliwa kwako na Roho Mtakatifu, nawe unaangalia hapa na ni ahadi katika Neno.

78 Sasa, uponyaji wa Kiungu ni ahadi katika Neno. Sasa, kama Roho Mtakatifu atakufunulia, ya kwamba Yeye amekufa apate kukuponya na sawasawa na kukuokoa, basi njoo ukiwa na matarajio ya kulipokea, naye Mungu bila shaka atahakikisha kwamba umelipata.

Sasa, unaweza. . .Huenda da—daktari akasema, "Sasa vema, achaneni nao. Halitawadhuru, nadhani. Watakufa tu kwa vyovyote vile."

79 Lakini ninyi kumbukeni tu, kama Mungu alifanya ahadi, wewe dumu pamoja nayo haidhuru hali ya mambo ikoje. Kama ukisema, "Vema, nina kansa, nina TB;" hilo halina uhusiano wowote nalo. Kama Mungu amelifunua, Mungu hutimiza ahadi Yake; hivyo tu.

80 Mara nyingi ninawazia kuhusu Yona. Nikiwazia juu ya dalili, watu huangalia dalili zao. Yona alikuwa na kisa halisi cha dalili. Alikuwa katika tumbo la nyangumi huku mikono na miguu yake imefungwa, naye alikuwa huko chini katika tumbo la nyangumi katika matapiko yote, na chini ya bahari, kwenye bahari yenye tufani. Sasa, alikuwa na dalili kweli. Kama aliangalia huku, ilikuwa ni tumbo la nyangumi; kule, ilikuwa ni tumbo la nyangumi; kila alipoangalia, ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Sasa, hakuna mtu hapa ndani aliye katika hali hiyo mbaya, nina hakika.

81 Lakini unajua yale aliyosema? Yeye alisema, "Ni ubatili udanganyao. Sitauamini." Alisema nini? "Mara nyingine tena nitatazama kukabili hekalu Lako takatifu."

82 Kwa kuwa yeye alijua ya kwamba wakati hekalu lile lilipowekwa wakfu, ile siku ambayo Sulemani aliliweka lile hekalu wakfu, yeye aliomba, na akasema, "Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida, mahali popote, nao wataangalia kwenye hekalu hili takatifu, basi sikia kutoka Mbinguni," naye alijua ya kwamba Mungu aliyasikia maombi ya mtu huyo.

83 Nanyi mnajua yale Mungu aliyofanya? Alimweka hai huko chini siku tatu usiku na mchana, akampeleka Ninawi, labda ilimchukua huyo samaki muda huo kuogelea kupitia majini, kumfikisha kule. Lakini alikaa kwenye tumbo la nyangumi siku tatu usiku na mchana. Alikuwa akimtarajia Mungu kufanya jambo fulani, kwa sababu alikuwa ametimiza matakwa. Mungu alikuwa amefanya ahadi naye akaiamini.

84 Basi ikiwa Yona, chini ya mazingira hayo, angeweza kupata mwujiza ukifanya kazi namna hiyo kutoka kwa Mungu, kwa sababu ilikuwa ni kulingana na Neno, ilikuwa ni kulingana na imani yake, na kama aliweza kufanya hivyo chini ya hali hizo za mambo, ni zaidi sana vipi, asubuhi ya leo, tunavyoweza kuponywa, wakati hatutazami kulikabili hekalu lililojengwa kwa mikono. Sulemani hatimaye alirudi nyuma, wake zake walimvuta wakampeleka mbali na Mungu.

85 Lakini tunaangalia mkono wa kuume wa Mungu ambapo Yesu ameketi pamoja na Damu Yake Mwenyewe, yu hai daima kutuombea tunapokiri. Ni zaidi sana vipi tunavyoweza kuita aina yoyote ya ugonjwa "ubatili udanganyao. Siuamini. 'Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu,

adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.' Basi, Shetani, chukua mkondo wako, toka hapa." Mnaona. "Ninamwamini Mungu. Ninalitarajia litukie." Haya basi.

86 Kama mimi. . .lisipotukia sasa hivi, litatukia baada ya kitambo kidogo. Lisipotukia leo, litatukia kesho. Lisipotukia kesho, litatukia juma lijalo. Chochote kile, litatukia kwa vyovyote vile. Mungu alisema hivyo. Haya basi. Sasa, unafikia mahali ambapo unaweza kupata imani. Kuwa ukilitarajia. Yale Mungu aliyosema Yeye angefanya, Mungu atayafanya. Hawezi kusema uongo.

87 Kwa hiyo Simeoni, aliyesifika sana, haileti tofauti yoyote kuhusu sifa njema. Hizo ndizo zimeyaingilia sana makanisa yetu siku hizi, hata kwa makanisa yetu ya Kipentekoste. Ni mtindo kupindukia, ninii nyingi kupindukia. . .za—za kipuuzi, kama vile tulivyo tu na sifa kuu, mwajua, na jamii, na kadhalika.

88 Tunachohitaji ni dini ya mtindo wa kale, ya huko nyuma misituni, ya anga za bluu, inayoua dhambi. Tunachohitaji ni Injili ya mtutu uliolenga vizuri, kitu ambacho kitaihubiri injili pasipo kupatana, na kuacha vibanzi vianguke popote vitakapo, na kuikatakata. Tunahitaji watu wa Mungu; wakikaa pamoja na nguvu, kulirudisha kanisa mahali ambapo linapaswa kuwa.

89 Kuna kasoro fulani. Tunatambua hilo. Sote tunajua hilo. Tunajua hilo. Makanisa yetu yanaanguka, yanakuwa dhaifu. Tunachohitaji si—si—si—si dhehebu jipya kuibuka, tunachohitaji siyo mvua nyingine ya vuli; kile tu—kile tunachohitaji ni kurudi kwenye imani katika Neno la Mungu na Biblia ya Mungu. Tukio linaloitikisa nafsi irudi kanisani, hilo ndilo tunalohitaji, kusafishwa, kunyoshwa, kote katika makanisa yetu na madhehebu yetu. Tuache kuweka mipaka midogo midogo; *hili* tu na *lile*.

90 Dhehebu fulani, hivi majuzi, kwa sababu kwamba nilimruhusu mhudumu mwingine aketi jukwaani ambaye hakuwa mfuasi wa shirika lao, yeye alisema, "Tumechora mstari. Tumekuweka nje yake, Ndugu Branham, nje ya—nje ya kundi letu."

91 Nikasema, "Ninachora mwingine, mkubwa sana, kuwarudisha ndani tena." Nikasema, "Kwa hiyo ha—hamwezi kunilazimisha nitoke nje." Hiyo ni kweli. "Nitachora mstari moja kwa moja juu ya huo wenu na kuwaingiza ndani moja kwa moja." Mnaona?

92 Hiyo ni kwa ajili ya. . .Sisi ni ndugu. "Hatujagawanyika; sisi sote ni mwili mmoja." Kweli. Sisi ni Wakristo, waliozaliwa kwa Roho Wake, tukaoshwa kwa Damu Yake. Sisi ni Wakristo. Inatupasa kutenda kama Wakristo; inatupasa kuenenda kama Wakristo. Wanaume na wanawake, hebu niwaambie hilo ni jambo moja sisi, kanisa limepungukiwa nalo siku hizi, ni

kuenenda kama Wakristo. Tunaenda huku na huku, tukitenda kama nzi waliokufa. Tunaenda . . . Ni la kuchukiza mno. Hakuna imani, si ya kutosha, kama ilikuwa ni wino, kuweka nukta ya "i." Kwa urahisi tu, tumepoteza kitu fulani. Tunachopaswa kufanya ni kuweka mabega yetu nyuma.

93 Miaka mingi iliyopita walikuwa wakiuza watumwa kwenye masoko ya watumwa huku kusini, sana sana huko chini Georgia, na kadhalika, wakati . . . Nao wangeenda juu ya . . . nchi za ng'ambo katika Afrika, nao Makaburu wangewarudisha watumwa. Wawalete huku nje Jamaika, na kuwapeleka kwa meli mpaka Florida, na kuwauza, wanadamu. Hilo lilikuwa ni kosa. Mungu alimwumba mwanadamu, naye mwanadamu akawafanya watumwa. Hakuna mtu anayepaswa kuwa mtumwa. Tuko huru katika Kristo. Sisi si mtumwa wa taifa lolote, si mtumwa wa dhehebu lolote. Sisi ni wanaume na wanawake wa Mungu. Tunainyosha mikono yetu kwa kila ndugu aliyeanguka, haidhuru yuko wapi. Ipo nafasi kwa ajili ya sisi sote. Kwa hiyo tunapofikia mahali . . .

94 Wao wangezunguka-zunguka, wawanunue watumwa hawa kwenye mashamba makubwa mbalimbali. Wangepata tangazo la mauzo, kama tu vile ungepata la gari la mtumba, kwenye uwanja wa kuegeshea magari, mahali fulani. Kwa hiyo wangezunguka-zunguka na kuwanunua hawa watumwa. Wangechukua . . .

95 Nilisoma kuhusu Abraham Lincoln, mkusini mashuhuri, aliyeshuka kwenye mtumbwi kule New Orleans, naye akawaona kwenye shimo la watumwa kule, wakimpiga mnada Mnegro mkubwa mno, shupavu. Naye maskini mke wake amesimama huko nje pamoja na watoto wawili, wakilia, kwa kuwa walikuwa wakienda kumwuza wapate kumzalisha kwa wanawake wakubwa zaidi, wenye afya wapate kuwazaa watumwa wakubwa zaidi. Abraham Lincoln akakunja ngumi yake namna *hiyo*, na kusema, "Hiyo si haki. Siku moja nitalipiga, hata ikinigharimu maisha yangu." Ilimgharimu maisha, bali aliipiga. Akaivunja, pia.

96 Hebu nikwambie, ndugu, kutokuamini ni kwa ibilisi. Hebu nikupige, Bwana. Sijali kama kukinigharimu maisha yangu. Nijalie kukivunjilia mbali kitu hicho juu ya kanisa, hiyo mipaka, na kadhalika, tupate kuona, sisi, kwa Roho mmoja, sote tumebatizwa kuwa mwili mmoja, nasi ni Wakristo. Sisi ni ndugu. Haidhuru kama huyo mtu ni mfuasi wa Church of God nami ni wa Assemblies, naye huyu ni Mbaptisti, ama Mpresbiteri; sisi ni ndugu, hivyo ndivyo tulivyo, sisi ni ndugu katika Kristo. Hebu tukivunje. Tuivunjilie mbali mipaka hii. Tunaweza kumnyoshea mikono yetu kila ndugu.

Nilikuwa hapa wakati mmoja uliopita, wao wakasema, "Ndugu Branham, laiti ungalijiunga na dhehebu letu."

97 Nikasema, "La, mimi niko pamoja na dhehebu lenu, bali nawaambia nitakalofanya: nitainyosha mikono yangu pande zote mbili kwa ajili ya kila mtu." Hiyo ni . . . Sisi sote ni mmoja katika Kristo.

Siku moja dalali huyu alikuja kwenye makazi ya shamba fulani. Akasema, "Una watumwa wangapi?"

Akasema, "Zaidi ya mia moja."

Kasema, "Ningetaka kuwaangalia."

98 "Vema." Wote walikuwa wakifanya kazi, nao walikuwa . . . walikuwa wana huzuni. Wange—wangefikia mahali ambapo wangejua ya kwamba kamwe hawatarudi kwenye nchi ya uenyeji wao tena, na kamwe hawatamwona Baba na Mama, wala hawatawaona watoto wao tena, na—na kadhalika, na wao—wao walikuwa na uzito mwingi wa moyo. Nao wangechukua mijeledi na kuwacharaza kuwafanya wafanye kazi; kuwafanya wavute na kufanya kazi, na lolote walilopaswa kufanya.

99 Siku moja wakati mnunuzi huyu wa watumwa alipokuja naye akaona vile alivyokuwa akiwacharaza hao watumwa, akiwafanya wafanye kazi, wote ila mvulana mmoja. Haikuwabidi kumcharaza mijeledi. Mabega nyuma, kidevu juu; alikuwa ameshika kazi wakati wowote.

Basi da—dalali huyo akasema, "Ni—ningetaka kumnunua jamaa yule."

"Loo," akasema mwenye mali, "hauzwi; siwezi kumwuza."

"Vema," kasema, "niliona haikubidi kumsahihisha."

Kasema, "La."

Kasema, "Kuna shida gani?" Kasema, "Yeye ndiye bosi wa hao wote?"

Kasema, "La, yeye ni mtumwa."

Kasema, "Labda unamlisha tofauti na unavyowalisha hao watumwa wengine."

Kasema, "La, wote wanakula katika manchani pamoja; wao ni watumwa tu."

"Vema," kasema, "ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao wengine?"

100 Akasema, "Nilishangaa pia, mpaka nilipogundua, siku moja, ya kwamba huko katika nchi ya uenyeji anamotoka, Afrika, baba yake ni mfalme wa hilo kabila. Na ingawa yeye ni mgeni, hata hivyo anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye anajiadibisha kama mmoja."

101 Loo, Mungu! Sisi ni wana na binti za Mungu, mwana wa Mfalme wa Mbinguni. Tutaenendaje basi? Maskini wanyonge, wanaosukumwa nyuma? La, bwana.

Baba yangu ni tajiri wa nyumba na mashamba,

Anashikilia utajiri wa ulimwengu mikononi Mwake!
Wa rubi na almasi na fedha na dhahabu,
Makasha Yake yamejaa, ana utajiri usiosemeka.

Kwa kuwa sisi ni mwana wa Mfalme!

102 Hebu tujiadabishe: Wanawake, msiwe kama walimwengu, msivalie kama walimwengu. Msiwe mambo haya ya kisasa, na upuuzi huu wote wanaofanya; kaeni mbali nao. Wewe ni binti wa Mfalme.

103 Waungwana, ninyi ndugu, haiwabidi kupigwa mkaangushwa na kusukumwa pembeni. Ninyi ni wana wa Mfalme. Naam, simameni, kisukumeni kifua chenu mbele, ikabilieni; ndivyo ilivyo bila shaka.

104 Tunamtarajia Mungu kutufanyia jambo fulani. Yeye hawezi kutufanyia jambo lolote wakati tukinyong'onyea huku kana kwamba sisi, kitu kilichokufa nusu. Yeye anataka kanisa changamfu. Anataka wa—washirika mle ndani wawe mawe yaliyo hai yaliyojengwa katika nyumba ya imani. Wanaomwamini, wanaomkubali, wakilichukua Neno Lake.

105 Sasa, mnasema, "Vema, nina sifa kubwa sana, Ndugu Branham. Mimi ni mfanyabiashara. Ninacheza karata kwenye shirika langu." Sijali una nini, ndugu, hakuna shirika kubwa zaidi duniani kuliko shirika la Yesu Kristo, wala kamwe hutajiunga nalo.

106 Unasema, "Vema, mimi ni mshirika wa kanisa." Kunalo Kanisa moja tu, Njia moja tu, Lango moja tu, hilo ni Yesu Kristo. Yeye aingiaye kwa njia nyingine yoyote ni kama mwizi na mnyang'anyi. Na kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili huo. Hiyo ni kweli nasi ni ndugu. Naam, bwana. Nasi ni wana na binti za Mfalme; inatupasa kujiadabisha. Sifa zetu si kitu duniani; vile zinavyotaka kuwa: Mbinguni, ambako tunataka m—msimamo wetu kuwa, mbele za Mungu.

107 Sasa, tunaona, tumfuatilie Simeoni . . . Ninaona nina yapata dakika tano zaidi. Hebu tumlete chini zaidi kidogo. Tunaona ya kwamba Simeoni alikuwa na sababu nzuri ya yale aliyokuwa akifanya, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa amemfunulia ya kwamba hataona mauti. Haidhuru nini, jinsi alivyokuwa ni mkongwe, ama chochote kulihusu, ni wengine wangapi waliokuwa wameshindwa katika kujaribu kumwona Yeye, lakini yeye, mwenyewe, kama mtu binafsi, alikuwa atamwona Kristo wa Bwana.

108 Loo, ndugu, dada, kama wewe—kama ungeweza kumfanya Roho Mtakatifu akufunulie sasa, "Mimi ndimi nitakayeponywa. Naam, bwana. Sijui yale hao wengine watakayofanya, bali utakuwa ni wakati wangu. Hii ndiyo saa ya kuponywa kwangu."

109 "Huu ndio wakati nitakaompokea Roho Mtakatifu. Mungu amenifunulia. Nami nitampokea." Ni tofauti, jambo fulani litatukia.

110 Kama vile "kilindi kikiita Kilindi, ngurumo za maporomoko ya maji Yako," alisema Daudi. Kwa—kwa maneno mengine, kama kuna kilindi *hapa* ndani kinachoita, hapana budi pawe na Kilindi *huko* nje cha kuitikia wito huo. Kwa maneno mengine, ni wangapi wanaoamini ya kwamba wewe—ya kwamba ungetaka kutembea karibu zaidi na Mungu? Inua mkono wako. Vema. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu ni Mponyaji? Inua mkono wako. Hakika. Vema, sasa, kama una kitu fulani ndani yako kinachokwambia hivyo, hapana budi pawe na kitu Fulani huko nje cha kuitikia shauku hiyo.

111 Hapa, namna hii: kabla hapajakuwapo na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi pawe na maji kwanza apate kuogelea ndani, la sivyo asingalikuwa na pezi. Kabla hapajakuwapo na mti wa kukua ardhini, ilibidi pawe na ardhi kwanza, la sivyo kusingalikuwako na—na mti wa kukua ndani yake.

112 Hapa siku moja . . . nilikuwa tu nikiwazia, nilinukuu hili hivi majuzi, kwamba m—mvulana mdogo jijini mwetu, alikuwa . . . alikula—alikula vifutio vyote kwenye penseli yake shuleni. Basi mwalimu akamwandikia mama yake. Ndipo mama yake siku moja, alimkuta nje kwenye kibaraza cha nyuma, akila pedali kutoka kwenye baiskeli. Kwa hiyo, ilikuwa ni raba. Na kwa hiyo wakamchukua wakampeleka kwenye maabara wakamchunguze maskini jamaa huyo wapate kujua shida yake. Ndipo daktari akakuta kwamba maskini mwili wake ulihitaji salfa. Sasa, unapata salfa katika raba. Sasa nini? Maadamu kulikuwako na shauku mle ndani kwa ajili ya salfa, ilibidi pawe na salfa kwanza. Ee ndugu, unaweza kuona ninalomaanisha? Ingebidi pawe na salfa *huko* nje kwanza, kabla hapajakuwapo na shauku *hapa* ndani. Mnaona?

113 Hiyo ndiyo sababu kuna Mungu zaidi kwa ajili yenu. Hiyo ndiyo sababu kunao uponyaji wa Kiungu kwa ajili yako, kwa sababu mnautafuta. Hiyo ndiyo sababu kulikuwako na Mungu ambaye . . . Ibrahimu alikuwa akiutafuta, ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu. Alikuwa akiutarajia, kwa sababu Mungu alikuwa amefanya ile ahadi. Mnaona?

114 Hapa, kabla hapajaweza kuwa na kiumbe, hapana budi pawe na Muumba kuumba hicho kiumbe. Na mradi tu unajisikia kwamba unaamini katika uponyaji wa Kiungu, kuna chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani. Mradi tu unaamini ya kwamba kunaye Mungu atakayekujaza na Roho Mtakatifu, kuna chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani la sivyo kamwe usingeweza kumwonea shauku. Wengine . . . Wengine wengi hawamwonei shauku, mnaona, kwa sababu haijafunuliwa kwao. Lakini imefunuliwa kwako. Kwa nini? Kwa kitu Gani?

Ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi. Mnaona? Ni kitu gani? Imefunuliwa kwako na Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu yeye yule aliyemfunulia Simeoni.

115 Na maadamu Yeye amelifunua, kuna chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani. Loo, laiti tungaliweza tu kuiona! Chemchemi imefunguliwa mahali fulani, kwa kuwa imefunuliwa kwako na Roho Mtakatifu, Mungu ni Mponya. Chemchemi hiyo iko wapi? Mungu hujaza kwa Roho Mtakatifu. Chemchemi hiyo iko wapi? Unaona kunayo chemchemi *huko* la sivyo usingekuwa na shauku hiyo moyoni mwako. Kwa hiyo linakufanya tu upoteze mawazo yako yote juu ya chochote kile, kwa sababu inapita kila kitu. Inajaza utu wako wote kwa kuliamini. Sasa, hakuna Roho Mtakatifu wawili. Kunaye Roho Mtakatifu mmoja tu, naye Roho Mtakatifu yule yule aliyemfunulia Simeoni amekufunulia wewe; kufunuliwa na Roho Mtakatifu.

> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Wenye dhambi wakitumbukia chini ya gharika
> hiyo,
> Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

116 Hiyo ni kwa ajili ya kila mwenye dhambi. Petro alisema kwenye siku ya Pentekoste kule, kasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii . . . " Loo, jamani! Unawezaje kuirudisha nyuma na kuiweka kwenye kitu fulani cha kihistoria? "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, kwa wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

117 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .? . . . Baraka za Kipentekoste, nguvu za Mungu zikijaribu kulichukua kanisa Lake; Yeye hakosei. Yeye hapungui. Yeye ni mwangavu na mpya tu leo hii kama alivyowahi kuwa, na daima atakuwa. Yeye ni wa Milele. Loo, naam.

118 "Wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu." David duPlessis wakati mmoja alisema juu ya hilo, kuhusu wana wa Mungu, "Wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu (Nyote mnaamini hilo, sivyo? "Wana, watoto wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu."), sasa, shida yake ni kwamba, kanisa siku hizi," akasema, "tunao wajukuu wengi kupita kiasi, bali Mungu hana wajukuu wowote."

119 Sasa, ninyi Wamethodisti, amkeni kwa dakika moja tu. Ninataka kulivua koti lenu. Kama tungali tulikuwa na wana na binti za Mungu wa Methodisti ingekuwa ni sawa. Kama tungalikuwa na wana na binti za Mungu wa Kibaptisti, ni sawa; Kilutheri, Kinazarayo, Pilgrim Holiness, ama Pentekoste. Lakini kama tu vile hao wengine walivyofanya, ndivyo nasi pia

katika Upentekoste. Tunawachukua watoto wetu na kuwaingiza kanisani, kwa sababu tulikuwa mle, tukiwafanya wafuasi wa kanisa la Kipentekoste; hao ni wajukuu!

120 Mungu hana wajukuu! Mwana yuyo huyo au binti hana budi kulipa gharama ile ile tuliyolipa, na kumpokea Roho Mtakatifu kama tulivyompokea sisi. Hakuna wajukuu. Mungu hawaingizi kwa. . .namna hiyo. Kunao wana na binti. Hakuna wajukuu, Mungu hana wowote. Hakuna kitu kama hicho kwa Mungu.

121 Vema, unasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa la Methodisti. Mama yangu alikuwa mle." Huyo ni mjukuu! Mungu hana hao! Wewe ni—wewe ni mjukuu kwa kanisa la Kimethodisti, wewe ni mjukuu kwa kanisa la Kipentekoste, bali Mungu hana wajukuu wowote. Kila mwanamume na mwanamke hana budi kuzaliwa mara ya pili kibinafsi, wana na binti za Mungu. Hilo ndilo linalowafanya wajawe na Roho na kujawa na uzima.

122 Msimu wa kuchipua unakaribia. Baada ya kitambo kidogo maskini ndege wote hapa wanaingia kwenye hiyo mipungate na vichaka huko nje, na kujijengea kiota. Maskini mama ndege anaweza kujenga kiota kidogo kizuri na kukifanya cha kupendeza sana kwa ajili ya watoto wake, atage kiota kizima cha mayai. Naye anaweza kuketi hapo juu ya hayo mayai, na mwaminifu sana, na kuyageuza tu sana, na kushikwa na njaa sana, naye atajinyima chakula, amedhoofika sana hawezi kuruka kutoka kwenye kiota. Kama mama ndege huyo hajawa na mwenziwe, hayo mayai kamwe hayataanguliwa. Hiyo ni kweli. Hayajarutubishwa. Mkondo wa damu hutoka kwenye jinsia ya kiume, ile himoglobini. Hiyo ni kweli. Mwanamke hutoa tu yai, jike, lakini kwa dume ndiko rutuba inakotoka.

123 Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu siku hizi. Watu wetu wa Kipentekoste. . .(Pasipo kusema chochote dhidi ya kanisa hili la ajabu na mchungaji wenu wa ajabu. Nilikutana naye, ninajua yale anayoamini.) Lakini siku hizi tunapata makanisa makubwa kuliko tuliyowahi kuwa nayo na imani yetu inapungua. Kuna shida gani? Mnaona, tunawaingiza wafuasi, wajukuu. Tunachohitaji, ndugu, sio. . .

124 Maskini ndege huyo, kama nisemavyo, angeweza kuketi pale, kiota hicho, mpaka awe amedhoofika sana asingeweza kuruka kutoka kwake. Lakini ikiwa hajawa na mwenziwe, mayai hayo yatafanya nini? Yatakaa papo hapo na kuoza. Unajua hilo kwa kuku wako. Yatakaa hapo na kuoza.

125 Kunalo jambo moja tu la kufanya, ndugu: kisafishe hicho kiota. Hiyo ni kweli. Hicho ndicho huduma zetu za Kipentekoste zinachohitaji leo ni wakati wa kusafisha kiota. Ondoeni mayai yaliyooza kwenye kiota. Kuingiza washiriki, na kuwafanya mashemasi na kadhalika, na kuwapapasa mgongoni kwa kuwa kidogo wanatoa sana kanisani; hawajui zaidi kumhusu Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Hiyo ni

kweli. Tunachohitaji ni tukio la kuzaliwa mara ya pili, pamoja na kurudi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na imani halisi ya kweli ya Kipentekoste kanis-. . . katika Mungu, ikifanya kazi kanisani mwetu. Hilo linaleta kitu fulani kwamba unaongozwa na Roho Mtakatifu. Wakati Neno linaponena, unasema "amina" Kwake, na unaliamini.

Simeoni akiongozwa na Roho Mtakatifu, na hapo alikuwa na ile Ahadi.

126 Sasa, katika kufunga huenda nikasema jambo hili. Hebu tuseme wakati unakuja . . . Habari hazikusafiri wakati huo kama zilivyofanya. Hebu mwangalieni maskini Mariamu, alikuwa akitarajia pia, bikira. Yeye angeninii . . . kamwe hakumjua mwanamume, bali Roho Mtakatifu alikutana naye na kusema, "Kitu hicho kitakatifu kitakachozaliwa ndani yako kitakuwa cha—kitakuwa ni cha Roho Mtakatifu. Mungu atakuwa ndiye Baba wa huyu Mwana."

Vema, yeye alimtarajia Mungu kutimiza Neno Lake. Hakuenda huku na huku akisema, "Sasa, ngojeni. Nitaona hata nitakapouhisi uhai ndipo nitaanza kushuhudia."

La, la. Sio vile unavyojisikia. Yesu kamwe hakusema, "Uliuhisi?" Alisema, "Ulililiamini?" Wewe liamini.

127 Mtu fulani anasema, "Vema, sijisikii tofauti hata kidogo." Hilo halina uhusiano nalo. Si kuzungumza kuhusu mkono wa nje na mwili wa nje: Anazungumza kuhusu sehemu ya ndani inayoliamini. Inaongoza hizo zingine.

Kasema, "Ulililiamini?"

128 Mariamu, mara Malaika alipomwambia, mbona, yeye alisema, "Tazama, mjakazi wa Bwana. Na iwe kwangu kama ninii Yako . . . sawasawa na Neno Lako." Akashika njia akapanda milima ya Yuda, akishuhudia. Akaenda akamwambia Elisabeti, binamu yake, ya kwamba atamzaa Mtoto, pasipo kumjua mwanamume yeyote. Mbona, Elisabeti alishtuka sana, kasema . . . Na mtoto Yohana, mwajua, alikuwa na miezi sita tayari, ameumbika katika tumbo la mama yake, hakuwa na uhai.

129 Yule Malaika mkuu akamtokea Zekaria, naye akalishuku Neno la Mungu. Akasema, "Utakuwa bubu mpaka wakati huyo mtoto atakapozaliwa." Mnajua, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Kama hutaki kulichukua, mtu mwingine atalichukua. Ndipo akasema . . .

130 Wakati, tunaona, alipomwamkua, yeye alisema, "Loo, Roho Mtakatifu atakuja juu yangu, nami nitapata mimba. Nacho Kitu hiki kitakatifu kitaitwa Mwana wa Mungu, nami nitamwita Jina Lake Yesu." Sasa, mtoto Yohana alikuwa na miezi sita pasipo kucheza. Mtu yeyote anajua hilo si kawaida. Miezi mitatu hadi minne sana sana halafu basi hapa ni miezi sita

wala hakuwa amecheza; bali mara aliposikia salamu hizo masikioni mwake kutoka kwa Mariamu, mwingine anayetarajia, mwingine anayetarajia, wote wawili. Ndipo wakati Mariamu aliposema . . . alipoliita Jina la Bwana Yesu, mara ya kwanza Jina hilo lilipopata kutajwa kwa midomo ya mwanadamu, maskini mtoto mchanga aliyekufa tumboni mwa mama yake aliruka kwa shangwe. Ndipo Yohana akampokea Roho Mtakatifu tumboni mwa mama yake na akaanza kuruka kwa shangwe.

131 Na kama mara ya kwanza Jina la Yesu Kristo lilipopata kutamkwa katika midomo ya mwanadamu ilimfanya mtoto mchanga mfu kuruka katika tumbo la mamaye kwa shangwe, linapaswa kufanya nini katika kanisa lililozaliwa mara ya pili, kupata imani kwa ajili ya nguvu za uponyaji!

132 Sijasisimkwa! Ninajua mahali nilipo. Mnaona? Lakini ninaanza tu kujisikia vizuri wakati mwingine ninapoanza kuzungumza juu ya mambo hayo. Mnaona? Hiyo ni kweli, kwa sababu ni kweli; Jina hilo la Yesu Kristo lina Uzima; na wakati linaponenwa kwa nguvu na imani, hakuna kitu kitakachosimama Mbele Zake. Hiyo ni kweli kabisa. Loo, hakika, wana na binti za Mungu.

133 Sasa, hebu tuseme Simeoni alikuwa ameketi huko nyuma katika chumba chake cha kusomea; labda ni Jumatatu asubuhi. Makuhani wote wako kazini mwao. Na kulikuwa na yapata Wayahudi milioni mbili na nusu huko Palestina wakati huo, kwa hiyo watoto kadhaa walizaliwa usiku kucha; kwenye siku ya nane watoto wa kiume ilibidi watahiriwe. Hebu tuwazie Simeoni ameketi huko nyuma ofisini mwake. Yeye analo Neno; analichunguza lote, namna *hiyo*. Ndipo analipata Gombo, labda hapa katika Isaya, Isaya 6:9. "Kwetu Mwana amezaliwa, tumepewa Mtoto," na kadhalika. "Ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa Milele." Ninaweza tu kumwazia ameketi pale.

134 Sasa, wakati wote maskini Mariamu alikuwa njiani akienda kule mtoto apate kutahiriwa. Anaingia kwenye mstari wa maombi, ama chochote kile, ule mstari unaoelekea kwenye tohara. Watoto wote walikuwa wamevalishwa nguo nzuri ndogo za kushonwa, mwajua. Nao jamaa wadogo warembo, na hawana meno, mwajua, na, loo, ninawapenda tu. Na kuwaona hao jamaa wadogo pale, na akina mama, wazuri, pamoja na mtoto wao mchanga; lakini hapa Yeye alikuwa . . . alifunikwa nguo Zake za kitoto. Mnajua walizitoa wapi? Kutoka kwenye nira ya maksai zizini, na hata hivyo ni Muumba mwenyewe wa mbingu na nchi! Nasi tunavaa suti ya dola hamsini na kuinua pua yetu juu, hivi, kama ingenyesha ingetuzamisha, naye Mwokozi wetu alizaliwa bila hata nguo za kumfunikia. "Mbweha wana matundu, ndege wa angani wana viota, bali Mwana wa Adamu hana mahali pa kuweka kichwa Chake." Kwani sisi ni nani? Inatupasa . . .?

135 "Vema, mimi...Mimi ni mfuasi wa kanisa lililo kubwa kuliko yote katika jiji hili." Loo, rehema, ndugu, dada, unapojisikia jinsi hiyo unamwondokea Mungu papo hapo! "Mungu anayo...Yeye anawajibika kwangu." Hawajibikii chochote. Wewe unawajibika Kwake. Ametekeleza sehemu Yake. Inakubidi kuamini kama tu hao wengine walivyoamini. Inakubidi kupitia njia ile ile waliyopitia.

136 Ninaweza kumwona Simeoni ameketi kule nyuma. Na mara sasa maskini Mariamu anaingia jengoni. Ninaweza kuwaona wanawake wengine wote wakimwondokea. Nadhani ninyi watu mliozaliwa mara ya pili mnajua ninalomaanisha. Alikuwa amesimama pale. Wanawake wanakaa mbali, kasema, "Mnamwona mwanamke yule pale...amempata mtoto huyo mchanga nje ya ndoa takatifu. Yeye na Yusufu ndio kwanza wafunge ndoa miezi michache iliyopita naye alikuwa tayari yuna mimba kabla hajazaliwa. Alikuwa—alikuwa na mimba kabla hajaolewa, hasa. Mnaona? Huyo ni mtoto haramu. Mwangalieni akimleta mtoto huyo haramu hekaluni mwa Mungu. Kaeni mbali naye." (Hivyo ndivyo waaminio halisi...) Lakini Mariamu, akimbeba maskini Mtoto huyo mikononi mwake, labda alikuwa ndani, nguo za kitoto zilizotolewa kwenye nira ya shingo, nira ya maksai horini. Labda ilikuwa, lakini moyoni mwake yeye alijua huyo alikuwa Mwana wa Nani.

137 Hivyo ndivyo ilivyo na kila mwaminio. Unajua huenda daktari akasema, "Loo, usiamini ulokole huo." Naye mama yako huenda akalisema, mume wako huenda akalisema, mke wako huenda akalisema, bali unajua wakati kitu Fulani kimezaliwa moyoni mwako. Mungu amekufunulia. Unatarajia jambo fulani kutukia.

138 "Usiende huko chini kwenye kanisa lile. Huna haja ya kwenda huko." Ni sawa. Utakuja vivyo hivyo tu wakati kitu Fulani kimo mle ndani. Mnaona? "Loo, hao ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha." Hilo halileti tofauti yoyote kile mnachowaita. Huenda ikawa...huenda...nguo zao za kitoto huenda zikawa ni za kawaida sana—sana, bali kwa vyovyote vile ninajua kilichofunikwa mle. Ninajua kile kilichofunikwa katika nguo za kitoto za Kipentekoste. Naam, bwana. Ninajua tuna kila kitu ndani yake, bali hata hivyo kunaye Roho Mtakatifu aliyefunikwa mle, pia. Ni kweli kabisa.

139 Akimbeba mikononi mwake namna *hii*, yeye hakujali yale hao wengine. Wote walikaa mbali. Wakati wowote unapompokea Roho Mtakatifu, umetiwa alama. Kila mtu, wanakutia alama. Wanajua, wao wanajua. Wanasema, "Ah, yeye ni mmoja wa hao watu wanaonena kwa lugha; anahudhuria kundi lile la Kipentekoste. Kaeni mbali naye. Msimwalike kwenye karamu ya karata." Msijali; yeye anaye Roho Mtakatifu asingeenda kwa vyovyote vile. Kwa hiyo—kwa hiyo haya basi, mnaona? Naam. Basi hapo, naona. Naam.

140 Baada ya kitambo kidogo, tunaona mle; na kila mmoja wao kidogo akicheka kichinichini na kuangua kicheko, mwajua, "Mnaona, yule ndiye. Yule ni mmoja wao. Pale pale, mnaona? Yule ndiye." Yeye alijua; hilo ni sawa, alikuwa akimshughulikia Mtoto wake. Yeye alijua Huyo alikuwa ni nani. Ilimaanisha mengi zaidi kwake kuliko mashirika yote na kila kitu kilichokuwako. Hao wote ambao hawakuamini, haikuwabidi kuamini, bali yeye angejua. . . alijua kile alichokuwa nacho. Hivyo ndivyo tulivyo. Tunajua kile tulicho nacho. Tunajua ahadi hiyo ni nini.

141 Sasa, Huyu hapa hekaluni, mara ya kwanza Mungu hekaluni Mwake, katika umbo la binadamu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Huyu hapa, maskini huyu Mtoto Yehova sasa, amekaa mikononi mwa mama yake. Maskini Jamaa huyu mdogo kama hao wengine, bali kulikuwako na tofauti hapo. Hiyo ndiyo tofauti, mnasena, "Vema, sisi huenda kanisani kama nyinyi," bali kunayo tofauti hapo (Mnaona?), wakati wowote unapofikia mahali pazuri, jambo lifaalo.

142 Huyu hapa anakuja akipitia jengoni. Sasa, kama Roho Mtakatifu amemfunulia hilo Simeoni, ni juu ya Roho Mtakatifu kuona ya kwamba Yeye—Yeye analitekeleza Neno Lake.

143 Drama kidogo hapa sasa: Simeoni yuko mle hekaluni, kule akiomba. Muda si muda mwajua, ni kitu gani kinachotukia? Wakati akiyasoma Maandiko hayo, Roho Mtakatifu anasema, "Simama, Simeoni!"

"Ni wapi. . . " siyo, "Unataka niende wapi? Unataka nifanye nini?" Hiyo siyo kazi; fanya yale Yeye aliyokwambia. Simama. Huyu hapa anakuja.

"Anza kutembea."

"Ninaenda wapi?"

"Haileti tofauti yoyote, endelea tu kutembea." Tembea!

Mnaamini wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu? Hawa hapa wanaanza kutembea.

"Kwani ninaenda wapi?"

"Haileti tofauti yoyote, endelea tu kutembea."

Anatoka nje, wanamwona mzee Simeoni akitokea mbele ya kusanyiko, anaangalia kote juu chini kule. "Nina—nina—ninaenda wapi, Baba?"

"Nenda tu hapa penye mstari huu mdogo wa wanawake, hapo chini, hao mamia kadhaa."

144 Huyu hapa anashuka moja kwa moja. "Nashangaa kuna nini?" Analibeba Gombo hili, Isaya, Kitabu, Gombo, Isaya 9:6, ameweka kidole chake juu yake, labda. Roho Mtakatifu hufanya mambo ya ajabu. Mnaamini hilo, ndugu? Mambo ya ajabu.

Huyu hapa anakuja akishuka chini. Muda si muda mwajua yeye anakuja moja kwa moja mahali maskini mwanamke huyu alipokuwa.

145 Sasa mnaona, hawakuwa na televisheni siku hizo, hawakuwa na redio na magazeti, ni kupashana tu mdomo kwa sikio. Wala hili halikuwa limetangazwa, Mtoto huyu alipozaliwa. Mnaona? Alikuwa tu. . . Yeye alikuwa. . . Vema, Yeye alikuwa ni wa kipekee kwa vyovyote vile. Hakuna mtu aliyekuwa ameliandika kwenye gazeti lolote. Kama lingalitukia leo hii, kamwe wasingeliliweka gazetini, isipokuwa wawe walitaka kukashifu ama kitu fulani.

146 Kwa hiyo hapa, akashuka, naye Simeoni akasimama papo hapo mbele yake. Basi alipoangalia pale. . . Unaona, ilifunuliwa kwake na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti mpaka atakapompata Kristo wa Bwana. Na kitu kile kile ambacho watu walikuwa wakidhihaki, Roho Mtakatifu alimwongoza moja kwa moja kwake. Hivi huamini Yeye alikuongoza hapa asubuhi ya leo vivyo hivyo, jambo lile lile, Roho Mtakatifu yule yule? Akamwongoza papa hapa. Alikuwa akitarajia kumwona huyu Kristo, naye huyo hapo akashuka; na mara alipomwona, akamtambua.

147 Sasa umekuja usiku wa leo. Umekuja; keti chini tu kama wewe unashuku, keti chini, jipe kiti. Angalia tu kwa dakika chache. Hivi unatarajia kumwona Yeye akiingia jukwaani usiku wa leo? Ninamtarajia. Unaona? Unaona? Ninalitarajia. Yeye atafanya hivyo, kama unalitarajia.

148 Na mara alipomwona, alipomwona huyo Mtoto, alinyosha mikono kwenye mikono ya mama akamtwaa huyo Mtoto, akamkumbatia moyoni mwake, na kusema, "Bwana, sasa mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, sawasawa na Maneno Yako, kwa kuwa macho yangu yameuona Wakovu Wako." Loo, jamani! Kuongozwa na Roho Mtakatifu!

149 Sasa, weka maneno haya moyoni mwako, na uangalie usiku wa leo uone wokovu wa Mungu. Nitasimama kwa dakika moja. Wewe weka hilo niani mwako; hebu Roho Mtakatifu akuongoze usiku wa leo kuuona wokovu wa Mungu. Yeye aliahidi angefanya hivyo katika siku za mwisho. Angalia kama Yeye anafanya hivyo. Mnaona? Kutarajia, leo hii tunayo matarajio makuu, kama yeye alivyokuwa nayo.

150 Na kulikuwako na mwingine siku hiyo aliyekuwa akitarajia. Nitamfikia wakati tu tukimalizia. Jina lake lilikuwa ni Ana. Yeye alikuwa nabii mke. Alikuwa hekaluni, kipofu; bali angeweza kuona kupita kuta za hekalu hilo.

151 Ninatumaini ya kwamba kila dhehebu lililojitenga leo hii linaweza kuona mbali zaidi ya kuta za dhehebu lako. Ni sawa, dhehebu lako, lakini ona mbali zaidi ya kuta zake. Unaona?

152 Wakati kipofu Ana alipoketi pale, mara. . .Alikuwa pia akitarajia faraja ya Israeli, bali alikuwa kipofu. Hapana shaka Roho Mtakatifu alimwambia, "Simama, Ana!" Akasimama. Huyu hapa anakuja, akizungukazunguka, akiongozwa na Roho Mtakatifu, kupitia kwa hao watu. Alifanyaje hilo? Alikuwa akitarajia, naye Roho Mtakatifu alikuwa akimwongoza; maskini mwanamke huyo kipofu, akiongozwa kupitia kwenye watu hao, akija. Huyu hapa Simeoni, machozi yakitiririka kwenye ndevu zake nyeupe kama theluji. "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani."

153 Ninashangaa vile huo umati uliocheka kichinichini ulivyowazia basi. Mnaona? Makelele haya yote yalikuwa ni ya nini? "Vema," wakasema, "huyo hapo Ana mkongwe; yeye ni kipofu. Na yule pale Simeoni; yeye ni mzee na kidogo amerukwa na akili."

154 Lakini walikuwa wamesimama mahali pafaapo. Haijalishi walikuwa katika hali gani, walikuwa wamesimama mahali pazuri. Hapo ndipo ninapotaka kusimama. Mungu, jalia nisimame mahali panapofaa!

155 Naye huyu hapa anakuja akizungukazunguka kupitia pale. Sasa, kama Roho Mtakatifu angeweza kumwongoza mwanamke huyo kipofu mkongwe kupitia kwa watu hao wote apate kumfikia Yeye, ni zaidi sana vipi Yeye anavyoweza kukuongoza kwenye mitaa hii usiku wa leo? Tunafikia mahali ambapo tunaamini Yeye atawaponya wagonjwa, atawaokoa waliopotea.

156 Naye huyu hapa anakuja. Na mara alipofika pale, yeye pia alipapata mahali hapo, akainua mikono yake na kumbariki Mungu na kunena habari Zake, na kunena habari za s-. . . mwiba utakaokuwa moyoni mwa Mariamu, na kadhalika, kisha akatabiri. Mnaona, alikuwa nabii mke, naye Roho wa Mungu alikuwa juu yake. Naye Mungu akamwongoza mwanamke huyo kipofu mkongwe kupitia kwa huo umati hata akafika mahali pale, kwa sababu alikuwa akimtarajia Yeye aje.

Ninamtarajia. Kama utakuwa ukimtarajia Yeye, Mungu atatimiza matarajio yetu.

157 Mwanamuziki mashuhuri sana, hapa tu miaka michache iliyopita, alienda huko Urusi naye alikuwa akicheza lele, naye alikuwa akicheza kwa ustadi sana mpaka Warusi walikuwa wakishangilia kwa sauti zao zote. Walisimama na kupiga makelele, na wakapiga mayowe, na kumshangilia apate kucheza mara nyingine moja tu. Nao. . .naye akasimama (sasa sikilizeni), nao wakasha-. . .wakapiga mayowe tena, na kukanyaga kwa kishindo, apate kucheza tena lele hii kuu.

158 Na yeye—yeye. . .Wakamwona huyu mvulana. Wakasema, "Hapana shaka amerukwa na akili. Haoni vifijo vyetu. Havioni. Tunajaribu kumwita arudi acheze tena." Lakini waliona alisimama tu namna *hiyo*, amekodoa macho. Kwa hiyo baada ya

kitambo kidogo wakageuka kuangalia, yeye hakuwa akivutiwa na kushangilia kwa hao watu; lakini maskini mwalimu wake, mzee bingwa wa muziki, alikuwa ameketi huko juu kwenye wasikilizaji, alitaka kuona yale aliyosema kuuhusu. Alitaka kujua kama angemshangilia, ama kutikisa kichwa chake amefanya vema. Yeye hakujali yale watu waliyosema; alitaka kujua yale yeye aliyosema.

159 Na kama watu wakikwambia ya kwamba siku za miujiza zimepita, Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele, usiangalie yale watu wanayosema, lakini angalia juu kwa Bwana Yule aliyeliandika hilo Neno. Elekeza macho yako huko juu, unaona, yale Yeye anayosema kulihusu. Kama uponyaji wa Kiungu ni wa kweli, litafute Neno Lake leo, na uje ukitarajia usiku wa leo. Tunaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja tu?

160 Bwana mwenye rehema, ninashukuru kwa ajili ya kusanyiko hili dogo ambalo limeketi hapa sasa, likingojea. Ninaomba ya kwamba Wewe utaingiza mbegu kadhaa mioyoni mwao, wapate kuja usiku wa leo wakiwa na matarajio makuu, hata viwete watatembea, vipofu wataona. Jalia kusiweko na mtu mmoja dhaifu miongoni mwetu usiku wa leo. Jalia matatizo yote ya moyo yaponywe, kansa. Na jalia Roho Wako ashuke chini, na hata kwenye makazi yao alasiri ya leo jalia waponywe kabla hata hawajafika kanisani. Tunatarajia, Bwana, mambo makuu.

161 Kwa hiyo waongoze watu katika nyumba ya Mungu usiku wa leo; mwongoze mwenye dhambi, mvulana huyo mtundu, kipenzi cha mamaye ambaye ameyapangusa machozi yake, naye yule pale ameketi sakafuni mwa baa leo hii; binti huyo mtundu, huko nje usiku kucha. Jalia Roho Mtakatifu anene na kuiongoza miguu yao kwenye nyumba ya Mungu kisha madhabahuni usiku wa leo wakampate Kristo, Mwokozi wao. Basi tujalie, kama Simeoni wa kale, kwa mikono ya imani, tumkumbatie Bwana Yesu wa thamani mioyoni mwetu usiku wa leo, na kuufanya moyo wetu kitanda kidogo. Jalia ujuzi wetu pamoja Naye uwe ni nguo za kitoto zitakazotufanya tuishi tofauti tangu sasa na kuendelea.

162 Mbariki maskini ndugu yetu mchungaji hapa, na wahudunu hawa wengine, na yeyote aliyeko—aliyeko kanisani, Bwana, leo hii, mbariki. Tukitumaini ya kwamba utalipa kila kanisa ibada kuu leo hii; jalia iwe ni siku ambayo hatutaisahau. Tudumishe wenye nguvu sasa kukutumikia Wewe. Wabariki hawa watu wanapoenda kwenye makazi yao. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

163 Ninapoirudisha ibada kwa mchungaji, samahani kwa kuwaweka kupitisha wakati. Ninajua nyinyi huondoka saa sita na ni saa sita na robo, lakini hilo kwa namna fulani ni dogo kwangu. Wakati mwingine ninapopata . . . Sijui wakati wa

kumalizia, unajisikia vizuri sana. Kwa hiyo wakati mwingine nipo hapa saa mbili ama tatu namna hiyo. Kwa hiyo ni—ninalipenda tu; na wakati kusanyiko linaloitikia vizuri kama hili, naja na matarajio usiku wa leo ya kwamba Mungu atatenda mambo makuu, ya ajabu kwa ajili yetu. Mpaka wakati huo, Mungu daima awe pamoja nanyi, ninapoirudisha ibada kwa mchungaji wenu, na asanteni mara milioni moja kwa kusikiliza, ninyi nyote.

61-0205M Tarajio
Central Assembly Of God
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org